

Chanjo za COVID-19: Jambo la Kujua

Je, naweza kupata chanjo wapi?



Napataje miadi?



Mhudumu wako wa afya

Pigia mhudumu wako simu au tafuta miadi mtandaoni



Kliniki za chanjo kwa umati

Tembelea tovuti yetu: vaccinelocator.doh.wa.gov/



Famasia za ndani

Au piga 1-800-525-0127, kisha ubonyeze #.
Usaidizi wa lugha unapatikana.



Kliniki za kutokea tu au kliniki za jumuiya

Inatofautiana. Unaweza kusikia kuhusu kliniki kutoka kwa rafiki au mwanachama wa jumuiya. Waulize jinsi ya kujisajili.

Nafaa kuleta nini kwenye miadi yangu ya chanjo?

Unaweza kuombwa mambo yafuatayo, lakini huhitaji kuyaleta:

- utambulisho
- kadi ya bima
- nambari ya usalama wa umma



Gharama ya chanjo ni gani?

Unapata chanjo bila gharama yoyote kwako. Hufai kutozwa ada au kutumiwa bili.



Je, nahitaji dozi ya pili?



Baadhi ya chanjo ni za dozi mbili. Inachukua karibu wiki mbili baada ya kupewa chanjo kamili ili kupata ulinzi zaidi. Baadhi ya watu wanawea kuhitaji dozi ya kiongeza nguvu.

Pfizer-BioNTech

dozi 2, umbali wa siku 21

Moderna

dozi 2, umbali wa siku 28

Johnson & Johnson

dozi 1



Huhitaji kuwa raia wa Marekani ili kupata chanjo. Hawatauliza hali yako ya uhamiaji. Data ya kibinasi itatumika tu kwa madhumuni ya afya ya umma.



Tembelea: COVIDVaccineWA.org au DOH.WA.GOV/Coronavirus



Piga: 1-800-525-0127, kisha ubonyeze #. Usaidizi wa lugha unapatikana.

Kwa maelezo zaidi

Vaccinate
WA

CovidVaccineWA.org

Kuna madhara gani?

Una uwezekano wa kuwa na madhara.

Kwenye mwili wako wote:

- Uchovu
- Maumivu ya kichwa
- Maumivu ya misuli
- Baridi kali
- Joto kali
- Kichefuchefu



Kwenye mkono wako katika eneo lililodungwa sindano:

- Maumivu
- Wekundu
- Kuvimba



Kwa chanjo zilizo na dozi mbili, madhara yanaweza kuwa mbaya zaidi baada ya sindano ya pili.

Piga simu kwa 911 ikiwa una mzio. Unaweza kujisajili kwa V-safe ili kuripoti madhara yoyote: vsafe.cdc.gov.

Je, chanjo moja ni bora kuliko nyingine?

Tunapendekeza chanjo ya mRNA ya COVID-19 (Pfizer-BioNTech au Moderna) badala ya dozi moja ya chanjo ya Johnson & Johnson (J&J).

Chanjo ya J&J bado inapatikana iwapo unataka kuipata. Ongea na mhudumu wa afya kuhusu chaguo zako.



Chanjo ya COVID-19 hufanya nini?




Chanjo ya COVID-19 hufunza mwili wako kujenga ulinzi dhidi ya ugonjwa ambao hukulinda dhidi ya kuwa mgonjwa.

Je, chanjo ni salama?

Ndiyo. Chanjo zote zilipimwa kwa **maelfu** ya watu.

Zilionyeshwa kuwa salama kwa watu wa uasili kadhaa na walio na hali za kiafyा kama kunenepa kupita kiasi, kisukari, ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa ini, na VVU.



Department of Health (Idara ya Afya) hukagua ripoti za usalama mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa hakuna wasiwasi wa usalama.

Ni kwa nini nafaa kupata chanjo?

Kupata chanjo kutakusaidia kuwa salama kazini na kuvunjari na marafiki zako na familia tena.

Utakuwa na uwezekano wa chini zaidi wa kuwa mgonjwa sana, kulazwa hospitalini, au kufa kutoptana na COVID-19.

